DOKEZO LA KISHERIA

13 Julai 2019

MABADILIKO MBALIMBALI YA SHERIA ZINAZOSIMAMIA ASASI ZA KIRAIA (AZAKI) TANZANIA: MAANA NA MANTIKI YAKE PAMOJA NA MAPENDEKEZO

1. Utangulizi

Mswada wa Mabadiliko Mbalimbali ya Sheria wa Mwaka 2019 (yaani, *the Written Law (Miscellaneous Amendments) Bill of 2019 (Act No. 3/2019)*) ulipitishwa kuwa sheria na Bunge na kuanza kutumika tarehe 1 Julai 2019 baada ya kusainiwa na Rais tarehe 30 Juni 2019. Sheria hii Namba 3 ya 2019 inarekebisha jumla ya sheria nane (8), ikiwa ni pamoja na Sheria ya Makampuni Sura ya 212; Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Sura ya 59; Sheria ya Jumuiya Sura ya 337; na, Sheria ya Usajili wa Wadhamini Sura ya 318. Hizi pia ndizo sheria kuu zinazoratibu kwa sehemu kubwa usajili na mwenendo wa Asasi za Kiraia (AZAKI) Tanzania Bara.

1.1 Taswira ya Jumla ya Mabadiliko ya Sheria

Mabadiliko ya sheria zilizotajwa hapo juu yana maana zifuatazo katika mfumo wa kisheria unaoratibu sekta ya AZAKI:

i. Kubadilika kwa vigezo vya kutambuliwa (mfano usajili) kwa AZAKI chini ya sheria mbalimbali (kuna mabadiliko ya tafsri ya 'kampuni', 'asasi isiyo ya kiserikali', 'jumuiya' na 'wadhamini').
ii. Wasajili na Mawaziri husika kuongezewa uwezo na wigo wa kimamlaka ya usimamizi na udhibiti.
iii. Kubadili hadhi ya usajili kutoka sheria moja kwenda sheria nyingine kwa baadhi ya AZAKI zilizoguswa na mabadiliko.
iv. Kuweka ukomo wa miaka kumi (10) wa uhalali au uhai wa Hati ya Usajili wa asasi zisizo za kiserikali. Ila, Hati ya Usajili inaweza kutolewa tena kwa kuiomba Ofisi ya Msajili wa Asasi Zisiyo ya Kiserikali.

1.2 Sheria ya Makampuni Sura ya 212

- Tafsiri ya Makampuni:
  - Maana ya makampuni yasiyo na hisa na yasiyofanya biashara ambayo inahusisha baadhi ya AZAKI, imebadilishwa na kutafsiriwa upya. Kwa sasa, shirika au taasisi itahesabika kuwa ni kampuni isiyo na hisa kama itakuwa inajihusisha na uwekezaji au shughuli za kibiashara; na, kazi nyinginezo kama ambavyo Waziri atabainisha kwa kadiri itakavyoamuliwa. Hivyo, kutokana

na mabadiliko haya, AZAKI ambazo zilikuwa zimesajiliwa chini ya sheria hii hazitaweza tena kufanya kazi kama taasisi zisizotengeza faida.

- Kuondolewa kwenye daftari la Usajili wa AZAKI zilizosajiliwa kama Makampuni yasiyokuwa na hisa:
  - Ndani ya miezi miwili tangu tarehe 1 Julai 2019, AZAKI zote zilizosajiliwa chini ya sheria hii kama makampuni yasiyo na hisa, zitakoma kufanya kazi.
  - Hata hivyo, kwa AZAKI zilizokuwa na Cheti cha Ukubalifu (*Certificate of Compliance*) zitahesabiwa kuwa zimesajiliwa chini ya Sheria za Mashirika yasiyo ya Kiselikali Sura ya 59. Sharti hili linahusisha asasi zilizosajiliwa hapa nchini na zile za kimataifa ambazo zilikuwa na usajili chini ya Sheria ya Makampuni.
  - Mabadiliko haya yanatakiwa kufanyiwa kazi na AZAKI husika ndani ya miezi miwili kuanzia tarehe 1 Julai 2019. Waziri anaweza kuongeza muda kwa AZAKI husika kuendana na masharti mapya ya kisheria.
- Uwezo wa Kufuta Usajili wa Makampuni:
  - Kifungu kipya (cha 400A) kimeongezwa katika sheria hii kumpa Msajili uwezo au mamlaka zaidi ikiwa ni pamoja na kufuta katika rejesta (orodha) kampuni yeyote ambayo, kati ya mambo mengine, imesajiliwa kiudanganyifu, inafanya biashara kinyume cha sheria au wanahisa au wakurugenzi wake wote wana marufuku ya kisheria kuingia nchini.

1.3 Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali Sura ya 59

- Tafsiri Mpya ya Asasi Isiyo ya Kiserikali (NGO):
  - Nyongeza katika tafsiri ya awali ni pamoja na maneno *'kukuza/ endeleza utawala bora, sheria na taratibu na haki za binadamu.'* Pia, kufuta katika tafsiri ya awali maneno *'kujitawala'* (*autonomous*) na *'maslahi ya umma'* (kwa kubadilisha na maneno *'ustawi wa jamii na umma'*).
  - Mashirika Madogo katika Ngazi ya Kijamii (*community based organizations - CBOs*) yametamkwa kuwa ni sehemu ya 'NGO' kuanzia sasa.
- Tofauti na AZAKI Nyingine:
  - Vigezo vya kukidhi kuwa Asasi Isiyo ya Kiserikali pia vimetofautisha AZAKI ambazo zipo chini ya mwavuli wa mashirika ya kidini au mashirika yenye kueneza imani, vyama vya wafanyakazi, klabu za michezo na vyama vya siasa, ambavyo hapo awali vilitambulika katika sheria hii kama Asasi Zisizo za Kiserikali.
- Uwezo wa Waziri:
  - Kifungu kipya kimeongezwa ambacho kinampa Waziri mwenye dhamana na Asasi Zisizo za Kiserikali mamlaka ya kutamka kuwa shirika lolote kutokuwa (na hadhi ya) Asasi Isiyo ya Kiserikali kwa mantiki ya sheria hii.
- Nyongeza ya Uwezo wa Kisheria kwa Msajili wa Asasi Zisizo za Kiserikali:
  - Kusimamisha kwa muda Asasi yeyote Isiyo ya Kiserikali ambayo inakiuka Sheria hii wakati madai au mashtaka dhidi yake yanafanyiwa maamuzi na Bodi ya Asasi Zisizo za Kiserikali.

- Kufanya ufuatiliaji na tathimini kila baada ya robo mwaka wa Asasi Zisizo za Kiserikali.
- Kupeleleza/Kuchunguza suala lolote dhidi ya Asasi Isiyo ya Kiserikali kwa kushirikiana na vyombo vya kusimamia sheria (ambavyo kwa Tanzania ni pamoja na Jeshi la Polisi; na, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)).

- Ukomo wa Kipindi cha Uhalali wa Cheti cha Usajili:
  - Muda wa Cheti cha Usajili wa Asasi Isiyo ya Kiserikali umewekewa ukomo wa miaka kumi (10) tu.
  - Hata hivyo, fursa ya kuomba tena Cheti hicho imewekwa kisheria kwa masharti kuwa:
    - Maombi ya kuomba tena Cheti yafanywe miezi sita (6) kabla ya muda wa Cheti kumalizika.
    - Bodi ya Asasi Zisizo za Kiserikali itajiridhisha kuwa, muombaji ametimiza matakwa ya usajili chini ya sheria hii na sheria nyingine.
- Nyongeza ya Masharti na Matwakwa ya Ukubalifu:
  - Sharti jipya la kusambaza kwa umma taarifa za ukaguzi wa hesabu – pamoja na kuwa zinawasilishwa katika Baraza na Bodi za Asasi Zisizo za Kiserikali kama ilivyokuwa hapo awali.
  - Msisitizo wa kuendana na misingi ya uwazi na uwajibikaji katika masuala ya kifedha kama ilivyobainishwa katika sheria nyingine.

1.4 Sheria ya Jumuiya Sura ya 337

- Tafsiri ya Jumuiya (za Kiraia):
  - Tafsiri ya hapo awali ya 'Jumuiya' imebadilishwa. Tafsiri mpya imeleta mabadiliko machache ambayo ni, kuondoa klabu, makampuni na ubia (*partnerships*) kutoka katika orodha ya Jumuiya zinazokidhi vigezo vya sasa. Kwa sasa pia, aina ya masuala ambayo Jumuiya inaweza kusajiliwa kisheria yametajwa katika sheria hii (zamani ilikuwa ni uhuru wa Wanajumuiya wenyewe kujiamulia kwa upana).
  - Vigezo vya usajili vimebadilishwa kidogo kutoka *'kwa muelekeo na malengo'* ya Jumuiya, na kuwa tu, *'ya kiuweledi, kijamii, kiutamaduni, kidini au manufaa ya kiuchumi au ustawi wa wanachama wake.'*
- Uhuru wa Kuendesha Shirika Kama 'Jumuiya' Nchini Tanzania:
  - Kifungu kipya kimewekwa katika sheria hii ambacho kinaondosha uwezekano wa mashirika (ya kimataifa) yaliyosajiliwa nchi za nje kufanya kazi Tanzania pasipo kwanza kusajiliwa upya hapa nchini.
  - Kabla ya mabadiliko haya, mashirikia hayo yaliruhusiwa kufanya kazi nchini bila kusajiliwa tena kwa masharti kuwa, watendaji wake au wanachama walikuwa wanaishi hapa nchini au mashirika hayo yalikuwa na wawakilishi wake. Kwa sasa hali ni tofauti; na, mfumo huu wa kisheria ni hivyo hivyo kwa usajili wa AZAKI zinazotoka nje ya nchi chini ya sheria nyingine.

- Uwezo wa Rais Kuamua Jumuiya ni Batili:
    - Kifungu cha 8 cha sheria hii kimerekebishwa. Marekebisho hayo yanathibitisha uwepo na uratibu wa mamlaka zaidi ya moja wa Jumuiya ambapo, Rais (wa Tanzania) ana uhuru wa kimamlaka wa kuamua Jumuiya yeyote kuwa ni 'batili' au ni 'hatari kwa utawala bora wa Tanzania.'
    - Mantiki ya tamko hilo la Rais ni kufutwa kwa usajili wa Jumuiya husika.
- Adhabu kwa Makosa Chini ya Sheria:
    - Mabadiliko ya kisheria yametambulisha adhabu kali zaidi dhidi ya wafanyakazi au mameneja wa Jumuiya ambayo imetamkwa kuwa ni batili.
    - Adhabu ya faini imeongwezwa kutoka *'isiyozidi shilingi za kitanzania 10,000'* na kuwa, *'isiyopungua shilingi za kitanzania 1,000,000 ila isiyozidi shilingi za kitanzania 10,000,000 iwapu mtu atapatikana na hatia ya uvunjaji wa maelekezo ya sheria hii.'*

1.5 Sheria ya Usajili wa Wadhamini Sura ya 318

- Tafsiri za 'Dhamana/ Amana' na 'Wadhamini':
    - Kifungu kipya kimeongezwa kutafsiri 'dhamana/ amana' (*trust*); na, 'wadhamini' (*trustees*). Maneno haya hayakuwa yametafsiriwa kisheria hapo awali.
    - Hakuna katazo lolote la kisheria kupitia mabadiliko haya. Hivyo basi, hadhi ya AZAKI au watu waliosajiliwa kama wadhamini , inabaki vilevile.

2. Mantiki na Maana ya Mabadiliko Haya kwa AZAKI Zote

Kwa kuzingatia aina ya mabadiliko yaliyofanywa katika sheria mbalimbali tajwa hapo juu, ambazo zinaratibu AZAKI hapa nchini, ni vyema wadau mbalimbali wakafahamu, wakaelewa, na kuchukua taadhari ya kiutekelezaji kwamba:

(i) Uhuru wa kusajili Asasi Zisizo za Kiserikali kupitia sheria mbalimbali haupo tena. Kwa sasa, kila shirika ambalo ni 'NGO' lazima likidhi masharti na liratibiwe chini ya Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali Sura ya 59.

(ii) AZAKI zilizosajiliwa chini ya sheria nyingine na kwa sasa zinafanya kazi za kijamii kama vile utoaji huduma, utetezi, ushawishi, maendeleo ya jamii ngazi za chini (mfano CBOs), na kadhalika, zina miezi miwili tu tokea tarehe 1 Julai 2019 kujiandikisha chini ya Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali Sura ya 59. Bila kufanya hivyo, zitakuwa zimejifuta kwa mujibu wa sheria.

(iii) Asasi Zisizo za Kiserikali za kimataifa ni lazima ziendane na matakwa ya sheria hizi kama hali ilivyo kwa AZAKI nyingine za hapa nchini.

(iv) Cheti cha Usajili wa Asasi Isiyo ya Kiserikali umewekewa ukomo wa miaka 10 tu kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

(v) Msajili wa Asasi Zisizo za Kiserikali kwa sasa ana nguvu (mamlaka) zaidi za kisheria kuratibu AZAKI zilizo chini yake ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathimini wa AZAKI hizo.

(vi) Kazi za Asasi Zisizo za Kiserikali kwa sasa zitakuwa zinafuatiliwa na kutathiminiwa kila robo mwaka na Msajili wa Asasi Zisizo za Kiserikali.

(vii) Mabadiliko haya ya kisheria hayajaweza kutatua suala la AZAKI kuwa na hadhi ya hisani (charity) ili ziweze kunufaika (moja kwa moja) na nafuu za kikodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hivyo basi, vyeti vya hadhi ya hisani (charitable status certificates) kwa minajili ya nafuu ya kodi, vitaendelea kutolewa na Kamishna wa TRA chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato kama ilivyo sasa – baada ya wahusika kupeleka maombi kwake.

3. Masuala ya Kuzingati Kuanzia Sasa

(i) Kufahamu kuwa, serikali kupitia kwa Msajili wa Asasi Zisizo za Kiserikali imeanzisha vituo vitano vya usajili katika ngazi ya kanda (Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Mwanza na Mbeya) ili kuharakisha mchakato wa AZAKI kufanya ukubalifu kwa mujibu wa vigezo vipya vya kisheria na kwa AZAKI mpya zinazotaka kujisajili.

(ii) AZAKI zinazotakiwa kujisajili au kutimiza masharti ya kisheria ya ukubalifu chini ya Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali Sura ya 59 zinahimizwa kutumia fursa hii mapema iwekezekanavyo.

Kuhusu Foundation for Civil Society (FCS)

Foundation for Civil Society (FCS) ni taasisi huru ya kitanzania isiyo ya kiserikali wala ya kibiashara, ambayo inatoa ruzuku na huduma za kujenga uwezo kwa asasi za kiraia (AZAKI) za kitanzania. FCS ilisajiliwa kama taasisi ya kisheria mwezi Septemba 2002 na ikaanza kazi mwezi Januari 2003. Katika kipindi cha miaka 17 kuanzia kuazwishwa kwake, FCS imeweza kuzijengea uwezo zaidi ya AZAKI 5,500 katika mikoa yote ya Tanzania, Bara na Visiwani, kwa kuzipatia mafunzo na ruzuku na hivyo kuzifanya AZAKI hizi kuwafikia zaidi ya wananachi milioni 31.

Kwa msaada au ufafanuzi kuhusu masuala katika dokezo hili, unaweza kuwasiliana na Idara Yetu ya Biashara, Maendeleo na Ushirikiano.

Idara ya Biashara, Maendeleo na Ushirikiano
Foundation for Civil Society
S.L.P 7192, Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255 754 005708
Barua Pepe: information@thefoundation-tz.org, Tovuti: www.thefoundation-tz.org